iii. Soksi jozi mbili nyeupe.
iv. Sweta yenye shingo ya V rangi ya kijani iliyoiva.
v. Aje na T-shirt moja (01) rangi ya kijivu, yenye kola nyeusi na nembo ya shule kwenye mfuko. Pia Tshirt zinapatikana Shuleni kwa Tshs 15,000/=.
vi. Sare ya Michezo ni track suti 01 ya dark blue yenye michirizi myeupe, koti lisiwe na kofia. jezi ya dark bluu (bukta na T-shirt) viwe na michirizi myeupe. soksi nyeusi na raba nyeupe.
vii. Viatu vyeusi pea 02 vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi pia kiwi nyeusi (dye nyeusi) na brush ya viatu;
viii. Nguo za kushindia ni sketi nyeusi ndefu zenye rinda box nane ziwe mbili na hiyo T-shirt ya kijivu iliyotajwa hapo juu.
ix. Gum boot kwa ajili ya matope vipindi vya mvua.

**N.B Kwa wanafunzi wanaovaa ijabu, aje na hijabu mbili nyeupe (kitambaa cha halua) kwa ajili ya darasani na hijabu mbili nyeusi kwa ajili ya kushindia ambazo ni ndefu za kufunika mikono. Zisiwe na mapambo ya aina yoyote.**

**kwa sare (uniform) zote atakazokuja nazo ziwe zimeandikwa (printed) majina yake mwanafunzi. Mwanafunzi yeyote asije na nguo za nyumbani.**

**3. MAHITAJI MUHIMU YA KUJA NAYO**

Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

i. Nakala ya cheti cha matokeo ya mwanafunzi ya kidato cha nne (form four result slip) na nakala (copy) ya cheti cha kuzaliwa cha mwanafunzi.
ii. Rimu mbili kwa kila mwaka – A4. Kwa muhula ni rimu moja (1)
iii. Shuka mbili (2), rangi ya bluu bahari, blanket moja (1) na chandarua rangi nyeupe.
iv. Vyombo vya chakula (kontena, kijiko na kikombe).
v. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko, dumu la lita tano (5) kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa pamoja na beseni la kufulia.
vi. **Lab coat.**
vii. **Kadi ya bima ya afya. (Mzazi jitahidi kumkatia mwanao bima ya afya ili kuepuka usumbufu wa gharama za matibabu akiwa shuleni)**
viii. Godoro moja (1) futi 2.5 kwa 6.
ix. Aje na vitabu vinavyohusisha masomo yake.
x. Scientific calculator kwa michepuo ya sayansi na hisabati na Graph pad 1.
xi. Dissecting kit kwa wanafunzi wanaosoma biolojia
xii. file kwa ajili ya kuhifadhia nyaraka zake mbalimbali za darasani.
xiii. Tochi ya solar kwa ajili ya matumzi yake ya kujisomea kipindi ambacho umeme unakata.
xiv. Sanduku la chuma (tranka) kwa ajili ya kuhifadhia vitu vyake.
xv. Nguo za ndani za kutosha, Taulo/kitenge/khanga bila kusahau nguo za kulalia (night dress).
xvi. Sabuni za kufulia na kuogea, vifaa vya usafi binafsi kama vile shavers pamoja na mahitaji mengine madogomadogo ikiwemo pesa ya matumizi ya mtoto (pocket money)

4. **Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 10 counter books na daftari 10 za msomi.
ii. Kwanja 1, jembe 1 na mpini wake, na reki 1 (kwa wanafunzi wa PCM)
iii. Hardbroom 1, softbroom 1, mfagio wa chelewa yenye mpini 1, na squeezer au mopper 1 (kwa wanafunzi wa PCB na PGM).
iv. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika kulingana na mtaala mpya.

